**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 15 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Taarifa ya Mwaka ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka 2005/2006 *(The Annual Report of The National Social Security Fund (NSSF) for the Year 2005/2006).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 411

**Madhara ya Dawa za Kulevya**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Watanzania wengi wanafahamu kwamba, dawa za kulevya kama mirungi, bangi na kadhalika, zinaleta madhara makubwa kwa afya za watumiaji wa dawa hizo:-

(a) Je, Serikali inaweza kuufahamisha umma wa Tanzania ni madhara gani yanayosababishwa na utumiaji wa dawa hizo?

(b) Je, kwa nini nchi jirani zimehalalisha utumiaji wa mirungi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dawa alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, yaani mirungi na bangi, zipo aina nyingi nyingine za dawa za kulevya kama vile *heroin, cocaine, opium compounds, amphetamines, mandrax* na kadhalika. Madhara ya dawa hizi yanategemea aina ya dawa inayotumika, njia ya matumizi, kwa mfano kuvuta, kumeza au kujidunga sindano, kiwango kinachotumika pamoja na muda wa matumizi ya dawa inayohusika. Kwa ujumla, madhara ya dawa za kulevya ni kama yafuatavyo: Kuchanganyikiwa akili; kupoteza kumbukumbu; kupunguza uwezo wa kufikiria; kupata madhara ya ini, figo, mapafu, kisukari, shinikizo la damu na kiharusi; kwa mama mwenye mimba, dawa hizo huathiri maendeleo ya ukuaji wa mtoto tumboni, mtoto anaweza kuzaliwa kabla ya wakati au akiwa mfu; kupunguza nguvu za kiume; kupunguza hamu ya kushiriki tendo la ndoa; kupunguza kinga ya mwili; kuharibika ngozi; kuwa tegemezi wa dawa kwa kila jambo; kujiingiza katika vitendo vya udokozi ili mhusika apate pesa za kununuliwa dawa; na kwa wale wanaotumia njia ya kujidunga sindano, mara nyingi wanashirikiana sindano na hivyo kuambukizana Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, hisia za awali anazopata mtumiaji wa mirungi na dawa nyingi za kulevya ni kupata hali ya kuchangamka na kujisikia kwamba, matatizo yanayomkabili yamekwisha. Hali hii ndiyo inayowavutia vijana kuanza kutumia dawa hizi na bahati mbaya jinsi anavyoendelea kutumia dawa ili apate hisia hizo, mahitaji ya dawa yanaongezeka, baadaye mtumiaji anaanza kuduwaa, kutoa mate ovyo, kuwa mgomvi na kusinzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani ya Kenya imehalalisha matumizi ya mirugi kutokana na sababu za kiuchumi na kijamii. Kenya ni moja ya nchi zinazosafirisha mirugi kwa wingi kupeleka Uingereza na nchi ambayo pia haidhibiti matumizi ya mirugi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la dawa za kulevya halina tofauti na tatizo la UKIMWI, je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba, kuanzia mwaka ujao tuwe na Siku ya Taifa ya Kupiga Vita Dawa za kulevya ili mada zitolewe na kusaidia kuelimisha watu kwa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, dawa zinaleta matatizo ya UKIMWI na kwamba nashauri kuwepo Siku ya Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kama mnavyofahamu, tayari sisi huwa tunaadhimisha siku hii Kimataifa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tumekuwa tukiadhimisha Siku ya Dawa za Kulevya tarehe 25 Juni kila mwaka. Kwa hiyo, tayari Serikali inaadhimisha siku ya dawa za kulevya ikiwa siku hii pamoja na mambo haya tunazungumzia, pia na masuala yote yanayohusiana na dawa za kulevya ikiwemo pia na maambukizi ya UKIMWI.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya nchi zimepiga vita dawa za kulevya kwa kuweka adhabu ya juu kabisa kwa waingizaji na wasambazaji wa madawa hayo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaonaje na sisi hapa Tanzania tuige mfano wa nchi hizo kwa kuleta sheria ambayo inapiga vita uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya na kuweka adhabu ya juu kabisa ambayo tunaweza tukaiweka katika nchi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kabisa kwamba, kunatakiwa kuwe na sheria lakini sasa hivi tunayo Tume ambayo ipo inafanya kazi hii, ambayo ni Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya. Kwa hiyo, sheria inakuja ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunaweka sheria kali ili wale wanaohusika na dawa za kulevya waweze kudhibitiwa.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watumiaji wa dawa za kulevya limekuwa ni jambo la kawaida kwenda kuwalaza katika hospitali za wagonjwa wa akili, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha vituo vya kuwafanyia ukarabati wa tabia hawa wanaotumia dawa za kulevya badala ya kuwalaza kwenye hospitali za wagonjwa wa akili, ambako pia wanaharibu tabia za wale wagonjwa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na ningependa nimpongeze Naibu Waziri wangu na kumkaribisha hapa Bungeni, akiwa ametokea kwenye matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wagonjwa wanaotumia dawa za kulevya ni wengi sana na wanalazwa katika hospitali za magonjwa ya akili. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya kwamba, hilo tumeliona na hivi sasa tunajenga Hospitali Maalum hapo Isanga, tumeanza mwaka jana kwa madhumuni hayo. Vilevile ningependa nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, tunayo Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, amesema tuweke adhabu kali lakini hakutaja ziwe adhabu za namna gani. Zipo adhabu na kama hakuridhika na hizo adhabu, basi atushauri ili tulete Muswada wa kwa kujaribu kupitia upya. Asante sana.

Na. 412

**Miradi ya Maji Vijijini**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, Benki ya Dunia ilikubali kusaidia Wilaya 50 kufadhili Miradi mbalimbali ya Maji Vijijini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Nzega; na kwa kuwa katika mwaka huu ukame ni mkubwa sana: Je, Serikali iko tayari kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo na kuongeza lengo la vijiji kuwa zaidi ya kumi kama ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Jimbo la Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2003, Serikali ilianza kutekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Wilaya tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika Wilaya hizi, idadi ya Wilaya iliongezeka hadi kufikia 12 mwaka 2004 na Wilaya nyingine 38 zilipangwa kuongezwa mwaka 2005 ili jumla ya Wilaya chini ya Mradi ziwe 50. Hata hivyo, kabla Mradi haujaanza kutekelezwa kwenye Wilaya 38 zilizopangwa kuongezwa, ambapo na Nzega ikiwa mojawapo, katika Kikao cha Bajeti cha mwaka 2005/2006, Serikali ilitangaza nia ya kubadili Mradi huu na kufanya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambayo itatekelezwa kwenye Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu mzuri wa kushirikisha Halmashauri zote, ulihitaji muda wa maandalizi. Maandalizi hayo ni pamoja na kuzungumza na washiriki wa maendeleo ili watenge fedha na kuweka taratibu na miongozo ya kutekeleza Programu hiyo. Maandalizi yamekamilika na utekelezaji wa miradi umeanza.

Kwa kuwa Programu hii itatekelezwa hadi mwaka 2025 ni wazi kuwa vijiji vingi zaidi vitapata huduma ya maji. Vijiji kumi ni vya kuanzia tu. Halmashauri zitakuwa na nafasi ya kuongeza vijiji vingine kadiri watakavyokuwa wanamaliza vijiji hivyo kumi vya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni kwa Halmashauri kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hii kwa ufanisi na wananchi kuibua miradi na kushiriki katika hatua zote za mradi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wananchi wa Wilaya ya Nzega, ambao wamekuwa na ahadi hii toka mwaka 2004 wamekuwa wakisubiri Serikali itatamka ni lini mradi huu utaanza kukamilishwa katika vijijini hivyo na katika majibu ya Naibu Waziri, bado hajasema ni lini ingawa amesema maandalizi yako tayari:-

(a) Je, anaweza akataja ni lini katika vijiji hivyo kumi, wananchi watapatiwa maji safi na salama kama ambavyo walikuwa wameahidiwa?

(b) Kutokana na ucheweshaji wa Mradi huu wa Benki ya Dunia na kutokana na wananchi wenyewe kuchanga fedha wakingojea miradi hiyo iweze kutekelezwa na Halmashauri za Wilaya zipo tayari kwa maandalizi ya kungojea fedha kutoka Serikali Kuu na kwa wahisani. Je, haioni kuchelewesha kukamilisha miradi ni kuwakatisha tamaa wananchi wenye kipato kidogo, ambao wamechangia fedha zao na kuziweka benki kwa

muda mrefu? Haoni kwamba anachelewesha na kukatisha tamaa wananchi wasichangie katika miradi mingine ya maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge ya kwamba, hii Miradi ya Nzega ambayo iko minne katika jimbo lake, ambayo kuna Nata, Upungu, Ndala na Nkimiziwa, itaanza muda si mrefu, kwani tulichokuwa tunasubiri ni fedha kutoka kwa mfadhili na fedha hizi kwa hivi sasa ziko tayari. Kulikuwa na taratibu nyingi sana ambazo zilikuwa za kukamilisha na napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu, taratibu zote hizo sasa zimekamilika. Kilichobakia ni mfadhili ambaye ni *World Bank* kutuingizia fedha katika akaunti ili ziweze kutawanywa katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili lilikuwa linahusu ucheleweshaji huu kwamba unakatisha tamaa wananchi ambao walichanga kwa nia moja na itawafanya washindwe kuchanga katika shughuli nyingine. Napenda kusema kwamba, ucheleweshaji huu haukuwa ni makusudi, Serikali imefanya hivyo bali ni taratibu ambazo zilitokana na wafadhili wetu, kama nilivyosema kwenye jibu la nyongeza la kwanza kwamba, imechukua muda mrefu. Taratibu zilikuwa ni nyingi sana na ndizo ambazo sasa tumekamilisha na nina hakika kabisa, punde fedha hizo zitafika na hatutazichelewesha mara moja tutazigawa kwenye Halmashauri zote husika.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika majibu mazuri ya Naibu Waziri, amesema kuna vijiji vinne ambavyo vitapata maji hivi karibuni vinavyotoka katika Jimbo la Nzega; na kwa kuwa Bukene iko katika Wilaya ya Nzega na katika Jimbo la Bukene kuna vijiji ambavyo viliahidiwa katika mradi huu, vijiji kama vile Sigili, Buhondo, Mahene na kadhalika; je, vyenyewe vitapata lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimwiwa Mbunge kwamba, wakati vijiji vya Jimbo la Nzega vinaanza kutekeleza mradi wake pia na Bukene watafanya wakati huo huo, kwani fedha zitapelekwa kwa ajili ya Wilaya nzima ya Nzega. Ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Jimbo lake, vijiji vifuatavyo ambavyo vitapewa mradi huo ni Nawa, Mahene, Buhondo, Itobo, Sigili na Ikindwa. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Kwa kuwa katika Wilaya ambazo zimenufaika na miradi hii ya Benki ya Dunia ni pamoja na Wilaya ya Mpwapwa; na kwa kuwa katika utekelezaji wa miradi hii ya awamu ya kwanza, Vijiji vya Chamanda na Igoji Kusini, Salaza mradi ulishakamilika na hivi sasa mabomba yalichukuliwa, wananchi wale wanapata shida hawana maji; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu hilo na atakuwa tayari kuwatembelea wananchi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini swali hili limekwenda Mpwapwa na Vijiji vya Mpwapwa ni vizito. Sasa kama unajua labda unapitapita huko, haya jibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, vijiji vya Chamanda na Salaza ni mojawapo ya vijiji vilivyopata huduma hii katika

awamu ya kwanza ya Wilaya 14 zilizopatiwa miradi ya maji. Napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge, pia napenda kuisisitiza Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ya kwamba, vijiji hivi kwa sababu mabomba yake yameng'oka kutokana na mvua, naomba kwamba sasa hivi waviingize katika programu hii na katika fedha ambazo zitapelekwa kwao katika awamu hii kwa njia ya *quick wins,* naomba hivi vijiji viwili navyo viingizwe ili waweze kumalizia hii miradi na kurudisha hali ya maji iwe salama. *(Makofi)*

Na. 413

**Uchimbaji wa Visima Virefu Kondoa Kusini**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Miradi mingi ya visima virefu imeshindikana katika maeneo mengi ya Jimbo la Kondoa Kusini ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Magasa, Mnjoja, Mwaikisabe, Madaha, Songolo, Haunai, Goima, Mirambo, Jangalo, Mlongia, Itolwa, Chorahu, Kinkima, Ombiri, Tumbakose, Hamelo na Gonga. Je, Serikali haioni kuwa, ni busara sasa kuchimba mabwawa katika vijiji hivyo, badala ya kuendelea kupoteza fedha kwa kuchimba visima virefu ambavyo havitoi maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kondoa, ipo katika nyanda kame hivyo, hutegemea sana vyanzo vya maji kutoka chini ya ardhi. Kutokana na maumbilie ya miamba ya maeneo hayo, ambapo maji hupatikana katika mipasuko ya miamba, upatikanaji wa maji kwenye maeneo ya aina hiyo huwa mgumu. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, utaotekelezwa katika vijiji kumi vya Wilaya ya Kondoa, unahusisha vijiji vya Magasa, Madaha, Mwaikisabe, Kidoka, Humekwa, Chase/Chinyika na Hamia (Jimbo la Kondoa Kusini) na Idindiri/Kisondoko, Itaswi/Kwadinu na Potea (Jimbo la Kondoa Kaskazini). Kati ya vijiji saba vya Jimbo la Kondoa Kusini vilivyochimbiwa Visima, visima katika vijiji vinne vya Kidoka, Humekwa, Chase/Chinyika na Hamia vina maji ambapo visima vya vijiji vitatu vya Magasa, Madaha na Mwaikisabe vimekosa maji. Mkandarasi ameteuliwa ili kufanya uchimbaji zaidi wa visima virefu katika maeneo mengine ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijiji vinane vya Kinkima, Goima, Jangalo, Mlongia, Itolwa, Songolo, Hamai na Churuku, ambayo ni sehemu ya vijiji vya Mradi wa Ntomoko, alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, vijiji vinne vya Kinkima, Hamai, Songolo na Vhuruku, vinapata maji baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kufanya matengenezo kwenye chanzo cha maji na baadhi ya maeneo ya Mradi huo na kuimarisha usimamizi wa Mradi. Vijiji zaidi vinaweza kupata maji baada ya matengenezo yanayoendelea kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ikikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Mrijo Juu, tayari kuna bwawa kubwa linalotoa huduma ya maji. Aidha, mwaka 2005 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, ilikamilisha ujenzi wa malambo kwa ajili ya vijiji viwili vya Ombiri na Mirambo. Vilevile, vijiji viwili vya Hawelo na Tumbakose, tayari vina visima ila mashine za maji zimechakaa na Shirika la *World Vision* limeonesha nia ya kusaidia vijiji hivyo katika ukarabati wa mashine hizo. Kijiji cha Gonga hakina huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, itafanya tathmini na kubaini teknolojia sahihi ya kuwapatia maji wananchi wa vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, ambao hawana huduma ya maji, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa kwa maeneo ambayo itashindikana kupata maji chini, itafanyika kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayoanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwaka 2007/2008. Mradi wa Mtaro wa Ntomoko ni miongoni mwa miradi itakayofanyiwa tathmini. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane kikamilifu na Halmashauri ya Wilaya ili kukipa Kijiji cha Gomba kipaumbele ili kiweze kufanyiwa tathmini hiyo pia.

**NAIBU SPIKA:** Jibu refu, swali la nyongeza liwe fupi kabisa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika majibu yake Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba, eneo ambalo nimelitaja la Jimbo la Kondoa Kusini lina ugumu sana wa kupata maji ya visima virefu; na kwa kuwa amekiri pia kwamba, Kijiji cha Mrijo Juu ambacho kina bwawa, kinahudumiwa vizuri sana na chanzo hiki; je, haoni sasa hakuna sababu ya kuendelea kuchimba visima virefu na hakuna sababu ya kufanya tathmini upya kwa sababu umeshafanya tathmini, tupewe miradi ya mabwawa makubwa ili tuweze kuokoa tatizo ama tuweze kutatua tatizo la maji katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba mambo ya maji ni vizuri yakifanywa kiutalaam. Kwa hali hiyo ni kwamba, ili tujiridhishe kwamba sehemu ina maji au haina maji ni vizuri tathmini ifanywe. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba, baada ya tathmini, kile kinachowezekana ikiwa ni bwawa au kisima ndicho ambacho tutakishughulikia fedha hizo zitakapokuwa tayari.

Na. 414

**Kucheleweshwa kwa Kesi za Kufaa**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kucheleweshwa haki ya mtu ni sawa na kumnyima haki yake:-

(a) Je, ni kwa nini kesi za Mahakama ya Rufani zinacheleweshwa sana?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa watuhimiwa wanaocheleweshewa hukumu wanapoonekana hawana hatia walipwe fidia kwa siku zote walizokuwa rumande?

(c)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.N.Y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phares K. Kabuye, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Rufani inaendesha shughuli zake za kusikiliza rufaa mbalimbali kwa kufuata utaratibu uliowekwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali halisi ya wananchi kuelewa haki zao, idadi ya kesi kwenye Mahakama mbalimbali hapa nchini zimeongezeka, zikiwemo rufaa zinazowasilishwa Mahakama ya Rufani. Ongezeko hili la kesi mahakamani halilingani na idadi ya Majaji waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, Serikali imeongeza idadi ya Majaji wa Mahakama ya Rufani kutoka tisa mwaka 2006 hadi 12 hivi sasa. Ongezeko hilo la Majaji wa Mahakama ya Rufani, limewezesha kuongezeka kwa vikao vya mahakama hiyo kutoka saba hadi 14 kwa mwaka. Aidha, kuhamia kwa Mahakama ya Rufani kwenye Jengo la Makao ya muda ya Mahakama, kunaiwezesha Mahakama ya Rufani kufanya vikao vitatu kwa wakati mmoja. Ni matarajio ya Serikali kuwa, rufaa nyingi zaidi zitasikilizwa na kuamuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtuhumiwa yeyote anaposhinda kesi na akiona ana haki ya kudai fidia, upo utaratibu wa kisheria wa kudai fidia hiyo Mahakamani na hivyo anaweza kufuata taratibu hizo kudai fidia.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi wamesoma na wengi wamechukua masomo ya sheria:-

(a) Kinachofanya Serikali isiajiri Majaji wa kutosha ni nini; ni fedha au kutokuwa na nia ya kusaidia wananchi wanaoteseka mahabusu?

(b) Kwa kuwa mimi kwetu kuna kijana ambaye alifungwa miaka 30 na ameomba rufaa ametoka baada ya miaka tisa, akakuta baba yake na mama yake wamekufa kwa janga la UKIMWI. Je, Serikali inaweza ikanipa uhakika kwamba huyu kijana anaweza akafanyiwa utaratibu angalau wa kusaidiwa maisha ambayo yamekwisha na amekuta mji umesambaratika? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vijana wengi kuchukua masomo ya sheria na kwamba wangepaswa kuteuliwa kuwa Majaji, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, si elimu tu inayofanya mtu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Kuna vitu vingi ambavyo

vinaangaliwa, uzoefu wa kazi, pamoja na maadili ya huyo ambaye anatakiwa kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufaa. *(Makofi)*

Pili, kuhusu huyo kijana ambaye alikuwa amefungwa kifungo cha miaka 30 na sasa hivi ameachiliwa. Napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo kwamba utakapokwenda Mahakamani ukaonekana huna hatia, hukutenda lile kosa, kinachotakiwa Mahakamani ni kuleta ushahidi unaothibitisha kosa, kama ule ushahidi haukuthibitisha kosa ndiyo unaonekana hauna hatia. Lakini ukweli ni kwamba, kuna watu ambao wametenda makosa lakini wanaachiwa kwa sababu hakuna ushahidi wa kutosha, ambao umepelekwa Mahakamani dhidi ya huyo mshtakiwa. Sheria ilivyo sasa hivi ni kwamba, lazima kosa lolote lile la jinai, lithibitishwe bila kuwa na sababu yoyote ile.

Sasa kama kuna mashaka yoyote yale yanayotolewa kwa faida ya mshtakiwa, kwa hiyo, kama ni faida iliyotolewa kwa mshtakiwa siyo kwamba hakutenda lile kosa. Inawezekana ametenda kosa lakini kulikuwa na mashakashaka fulani, ambayo yalimfanya Mheshimiwa Jaji aone kwamba, kweli ushahidi uliopelekwa dhidi ya huyo mtu, haukuwa unatosha kuthibitisha hilo kosa ambalo alishitakiwa nalo Mahakamani. Kwa hiyo, sikubaliani naye kwamba, huyo aliyefungwa miaka 30 na kuonekana hana hatia na Mahakama ya Rufaa sisi Serikali tutatafuta mpango wowote wa kumshughulikia ili maisha yake yawe mazuri zaidi. *(Makofi)*

Na. 415

**Sensa ya Mifugo Nchini**

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.N.Y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muhimu kujua idadi ya mifugo yote nchini na kwa kuwa Sensa ya Mifugo inayotumika kwa sasa ni ya mwaka 1988 ambayo imepitwa na wakati. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kupata takwimu *(data)* sahihi ili zitumike wakati ujao kuliko kuendelea na takwimu za zamani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali alilouliza Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Longido,kama ifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Naomba mpunguze mazungumzo, *Order in the House*, punguzeni mazungumzo mnayoyafanya. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni muhimu kuwa na takwimu sahihi za idadi ya mifugo yote nchini ili kuwezesha kupanga, kuratibu na kutoa maamuzi mbalimbali ya namna ya kutumia rasilimali hii ya mifugo. Kwa kuzingatia umuhimu wa takwimu hizo, urejeaji wake na watumiaji mbalimbali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*(National Bureau of Statistics)*, imepewa dhamana ya kusimamia na kuratibu ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu mbalimbali kwa wadau, zikiwemo takwimu za mifugo. Wizara yangu inashirikiana na Ofisi hiyo na wadau wengine kupata takwimu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kupata ushauri wa kitaalamu juu ya kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitumia utaratibu wa kufanya *survey*, sensa ya sampuli ya kilimo *(National Sampling Census of Agriculture)* na utaratibu wa kuhesabu mifugo yote *(Total Livestock Counting)* katika kukusanya na kupata takwimu sahihi za mifugo.

Sensa kamili ya mifugo ilifanyika mara ya mwisho mwaka 1984, kwa kuhesabu mifugo yote nchini. Sensa hii ilifuatiwa na ile iliyofanyika kwa njia ya kuhesabu mifugo kwa kutumia sampuli *(Sample Counting)* mwaka 1993/1994 hadi mwaka 1994/1995. Aidha, kuanzia mwaka 1996/1997 hadi mwaka 1998/1999, chunguzi za kila mwaka zilifanyika kupata takwimu za kilimo na mifugo.

Sensa nyingine ya sampuli ya kilimo ambayo ilihusisha mifugo ilifanyika mwaka 2002/2003. Hivyo, kuanzia mwaka 1984 hadi mwaka 2003, sensa ya mifugo imekuwa inafanyika kwa taratibu mbalimbali kama nilivyoeleza. Ni kweli kwamba, chunguzi hizo zinahusisha maeneo na vijiji vichache na hivyo kufanya takwimu chache za mifugo zikusanywe, ikilinganishwa na haja ya kupata takwimu za idadi ya mifugo kwa kuihesabu yote. Aidha, kwa kuzingatia muda kati ya vipindi vya sensa hizo, pamoja na mfumo wa mtawanyo na uzalishaji wa mifugo nchini, kunahitaji kubwa la kufanyika kwa sensa kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali wa kupata takwimu sahihi za mifugo kwa njia ya kuhesabu mifugo yote, unajumuisha kufanya maandalizi na hatimaye kufanya sensa yenyewe. Ili tuweze kufanya sensa kamili kama ile ya mwaka 1984, kiasi cha shilingi bilioni tisa zinahitajika. Kiasi hiki cha fedha ni kikubwa na Serikali haina uwezo wa kupata fedha hizo kwa sasa.

Hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, itaendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za mifugo, kwa kutumia matokeo ya sensa ya kilimo na mifugo ya sampuli ya mwaka 2002/2003 hadi hapo tutakapopata fedha za kutosha na kufanya hesabu za mifugo yote nchini. Wizara yangu tayari imeweka mpango wa sensa ya mifugo katika mpango mkakati kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 - 2009/2010 na jitihada za kutafuta fedha hizo zinaendelea kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa utaratibu wa Taifa letu ni kufanya sensa ya watu kila baada ya miaka kumi, labda itokee kwamba Taifa halina pesa za kutosha kufanya sensa hiyo, lakini utaratibu ni kila baada ya miaka kumi.

Je, kwa nini sensa ya mifugo isifanyike kila baada ya miaka kumi au 15 ili kuendelea kuwa na takwimu sahihi?

Pili, kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu mwaka jana, mifugo iliathirika sana kwa maana ya kwamba, mifugo ilikufa kwa wingi sana. Je, bado tunashikilia nafasi ya tatu Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan kwa wingi wa mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, pengine ingekuwa ni vizuri kufanya sensa ya mifugo kila baada ya miaka kumi au 15 ikioanishwa na ile sensa ya watu. Serikali inaangalia uwezekano wa aina mbalimbali kama nilivyoeleza na pindi utaratibu muafaka utakapopatikana, tutafanya hivyo, lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni azma ya Serikali kuona kwamba, kipindi hiki mpaka 2010 tunafanya sensa ya mifugo yote nchi nzima.

Swali la pili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, pamoja na ukame uliojitokeza mwaka jana, ambapo ni chini ya asilimia moja ya mifugo iliathirika na ukame huu, Tanzania bado ni ya tatu kwa idadi ya mifugo Afrika.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna minada kule Wanging'ombe na Saja ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuiimarisha ile minada iliyoko Saja na Wanging'ombe katika Wilaya ya Jombe ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Swali la msingi lilikuwa linasema takwimu za mifugo, sasa hii ni minada; Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kujibu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuahidi Mheshimiwa Yono S. Kevela kuwa, tutakuja Iringa ili kuona hali halisi anayoizungumzia ili minada hii iweze kutumika kikamilifu kama haitumiki kikamilifu, kama ambavyo tunafahamu kuwa inatumika kikamilifu.

Na. 416

**Ziara nje ya nchi kwa wafugaji nchini**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Serikali inatumia fedha nyingi sana kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira na athari zake katika maeneo mengi nchini ambao kwa kiasi kikubwa umechangiwa na ugumu wa wafugaji wengi kutoamini na kukaidi kuwa ufugaji wa kisasa katika eneo dogo linalolingana na uwezo wa kulisha mifugo yao, utanenepesha na kuboresha zaidi mapato yao, kuliko kuchunga mifugo yao nchi nzima na kwa kuwa methali isemayo tembea uone ni ya busara sana:-

(a) Je, si vyema sasa Serikali iwaandalie wafugaji wa kawaida wanaotokana na jamii za Kimasai, Wasukuma na Wamang'ati, ziara nje ya nchi yetu kama zinavyoandaliwa ziara za mafunzo nje ya nchi kwa Wabunge ili nao wakajionee wenyewe jinsi wafugaji wadogo wenzao wa Botswana, Zimbabwe na Lesotho wanavyofaidika na ufugaji wa kisasa na namna wanavyohifadhi mazingira ya nchi zao?

(b) Je, Serikali haitambui kuwa, mafanikio ya ziara za wafugaji husika nje ya nchi zinaweza kuharakisha kasi yao ya kuaminika, kuelewa na kuyakubali maagizo ya Serikali, jambo ambalo litapunguza kasi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchungaji holela na kuokoa gharama kubwa za kuyakarabati mazingira, ambazo zitaongezeka zaidi endapo wafugaji wataendelea kukaidi maagizo ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Serikali yetu inatumia kiasi kikubwa cha fedha katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na athari zake katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na vitendo vya binadamu visivyozingatia hifadhi ya mazingira kama vile uchomaji moto, ufyekaji misitu, kuchunga mifugo mingi katika eneo dogo na hivyo kusababisha mmomonyoko wa nchi au kulima kwenye vyanzo vya maji na katika maeneo yenye miinuko mikali bila kutumia matuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia kwamba, uharibifu huu wa mazingira kwa kiasi fulani tu unachangiwa na ufugaji lakini usiozingatia maelekezo ya kitaalamu ambao ni pamoja na kuwa na idadi ya mifugo isiyolingana na uwezo wa malisho na hifadhi ya vyanzo vya maji katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara yangu inatoa mafunzo ya ufugaji bora katika vyuo vya Mafunzo ya Mifugo vilivyopo Buhuri (Tanga), Tengeru (Arusha), Morogoro, Mpwapwa, Madaba (Songea) na Mabuki (Mwanza). Takriban wafugaji 1,600 wanapata mafunzo ya muda mfupi ya wiki mbili katika vyuo hivyo kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, inaandaa miongozo ya kutoa Huduma za Ugani kwa jamii ya wafugaji ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji kwa njia ya redio, semina, machapisho mbalimbali na kutoa ziara za mafunzo kwa wafugaji kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine. Ili kupanua huduma hiyo, kuanzia mwaka 2006/2007, Wizara yangu imelenga kutoa mafunzo kuhusu ufugaji bora kwa wafugaji 20,000 kila mwaka, ambapo mwaka huo wafugaji 20,440 walipatiwa mafunzo hayo katika vyuo vya mafunzo ya mifugo vilivyo chini ya Wizara yangu, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, vilivyoko katika Halmashauri za Wilaya na pia kwa vikundi vya wafugaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wafugaji ni dhana muhimu katika kutoa mafunzo. Changamoto kubwa ya ziara za aina hii na hasa za nje ya nchi ni gharama kubwa, kwa sababu zinawahusu wafugaji wengi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Wilaya zinaweza kupanga ziara za aina hii kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP),* chini ya eneo la kuwawezesha wafugaji kufuga kisasa. Katika kutekeleza hili, Wizara yangu itashirikiana Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Vikundi vya Wafugaji na Vyama vya Hiari vinavyosimamia maendeleo ya wafugaji ili kuona uwezekano wa kufanyika kwa ziara hizo.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na majibu hayo, naomba uniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ili kuwahamasisha wafugaji wabaki katika maeneo waliyotengewa, Serikali imechukua hatua gani za kuwawezesha kupata vifaa na nyenzo kwa gharama nafuu vya kukata majani nyakati za masika na kuyahifadhi kwa malisho wakati wa kiangazi?

Swali la pili, kwa kuwa nchi yetu inazalisha *molasses* katika viwanda vya sukari nchini, je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuwawezesha wawekezaji na kuwawekea mazingira yanayovutia ili kupanua ujenzi na uzalishaji wa vyakula vya mifugo ili kuwafanya wafugaji wabaki katika maeneo hayo kuzidi kulisha mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wizara yangu imekuwa ikitoa mafunzo kwa wafugaji wadogo wadogo takriban 1,600 kila mwaka. Mafunzo haya yanajumuisha pamoja na kilimo cha malisho ya mifugo, ambapo hifadhi ya majani au malisho kwa ujumla kuanzia kilimo, ukataji na utunzaji yanatolewa.

Pili, kuhusu uzalishaji wa *molasses* na kutumia kwa wafugaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wafugaji tayari wanafahamu aina mbalimbali za chakula cha mifugo, ikiwa ni pamoja na mabaki ya mazao kutoka kwenye viwanda ikiwemo *molasses* kutumia kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo, ambapo tayari kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga ndiyo ulikuwa wa kwanza kutumia mabaki ya pamba, wakijumuisha pia na *molasses,* lakini pia elimu kama hii imesambaa nchi nzima na kwa hiyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, tayari wazalishaji na wafugaji wako kwenye umoja huo wa kutumia rasilimali hii kwa ajili ya ustawishaji wa mifugo.

Na. 417

**Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2008**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa mara baada ya Uchaguzi wa 2005, Mheshimiwa Rais aliitaka *TFF* kuhakikisha kuwa Tanzania inashiriki kwenye Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika ya 2008:-

(a) Je, Serikali imeanza kuchukua hatua gani za kutimiza ari hiyo?

(b) Je, Tanzania itajipima kwenye mashindano gani ikiwa inajiandaa kwa mashindano hayo?

(c) Je, Serikali inajitosheleza na walimu waliopo katika kutimiza azma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Jimbo la Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hatua iliyochukuliwa na Serikali ni mchakato mzima wa kumtafuta kocha wa Timu ya Taifa *(Taifa Stars)*, kupitia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)*. Shughuli hiyo ilishafanyika kwa umakini sana hadi akapatikana kocha wa Timu ya Taifa wa Mpira wa Miguu, *Taifa Stars*, ambaye anatoka Brazil, kwa jina anaitwa Marcio Maximo. Kocha wake Msaidizi Itamori, ambao walifika hapa Bungeni mwaka jana, kama mnakumbuka, wakatambulishwa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, kocha huyo pamoja Msaidizi wake, walianza mara moja kazi ya kuinoa *Taifa Stars*, pia Kamati Maalum ya Saidia *Taifa Stars* ishinde iliundwa, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohammed G. Dewji, Mbunge wa Singida Mjini.

(b) Shirikisho la Soka Tanzania *(TFF)*, liliandaa ratiba ya michezo ya kirafiki ya kimataifa ili kujipima nguvu na kupata uzoefu zaidi. *Taifa Stars* ilicheza michezo ifuatayo katika kutimiza nia hiyo ya kujinoa vizuri:-

| | |
|---|---|
| *Taifa Stars VS Rwanda* | *Taifa Stars* 1 - Rwanda 0 |
| *Taifa Stars VS Harambee Stars Kenya* | *Taifa Stars* 0 - Harambee 0 |
| *Taifa Stars VS Angola* | *Taifa Stars* 1 - Angola 1 |
| *Taifa Stars VS DRC* | *Taifa Stars* 2 - DRC 0 |
| *Taifa Stars VS Uganda The Cranes* | *Taifa Stars* 1 - *Uganda the Cranes* 1 |

Vilevile *Taifa Stars* ilifanya ziara ya kimafunzo nchini Brazil kwa muda wa wiki tatu. Hivi sasa ninapojibu swali hili, *Taifa Stars* ipo Denmark kwa ziara ya mafunzo. Huko kote wamecheza na watacheza michezo mbalimbali ya kujipima nguvu na timu ambazo zina ujuzi zaidi. *(Makofi)*

Aidha, katika mchakato mzima wa kutafuta nafasi ya kucheza michezo ya fainali za Kombe la Mataifa Huru ya Bara la Afrika mwaka 2008, *Taifa Stars* imekwisha cheza michezo kadhaa katika kundi lake na ipo katika nafasi nzuri. Kwa sasa imebakiza mchezo mmoja tu kati yake na Timu ya Taifa ya Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge, Wafadhili, wadau na wananchi wote, wazidi kuipa *Taifa Stars* misaada ya hali na mali ili washinde mchezo huo na kusonga mbele kwenye michezo ya fainali nchini Ghana mwaka 2008.

Serikali haijitoshelezi na walimu waliopo katika kutimiza azma hiyo na ndiyo maana inaagiza kocha na kutafuta walimu kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia *TFF* inawatumia wataalamu hawa wachache, kuwafundisha walimu wazalendo kwa lengo la kupata wataalamu wengi zaidi hapa nchini. Aidha, Chuo cha Malya cha Maendeleo ya Michezo, ambacho kiko Mkoani Mwanza, kinaendelea kutoa mafunzo ya stashahada ya michezo mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu wa michezo hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Michezo, kwa jawabu lake sahihi katika swali langu la msingi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, amesema hivi sasa walimu kutoka nje au kutoka Brazil wanatoa mafunzo kwa walimu hapa nchini. Serikali haioni kwamba, sasa kuna haja ya kuwatafuta walimu wa hapa nchini nao wakaenda nje kujifunza zaidi ili baadaye wakaja kuchukua nafasi hizi za walimu wageni?

Lakini pili, hivi sasa Serikali inatumia fedha nyingi sana kuhudumia Timu ya Taifa; Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba sasa umeshafika wakati kuiomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, kuwe na Mfuko Maalum utakaochangiwa na wananchi wenyewe kwa ajili ya Timu ya Taifa ya Tanzania ili kuweza kuihudumia vizuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba, tuna wachache katika nchi yetu na ni vizuri Serikali ikawa na mkakati wa kutumia walimu wetu hapa hapa nchini. Mpango huo na mkakati huo upo Serikalini, kwa kupitia chama chenyewe kwanza *TFF* wana programu zao, *FIFA* pia wana programu ambayo wanatusaidia kupata walimu katika ngazi mbalimbali; walimu wa awali, walimu wa kati na walimu wa *advanced.* Pia Serikali ina mkakati mzuri tu kwa kutumia mikataba yetu ya kitaifa na ushirikiano wetu na nchi mbalimbali kama Ujerumani, kupeleka baadhi ya Walimu. Hivi ninavyozungumza, baadhi ya walimu wapo katika mafunzo mbalimbali katika nchi ya Ujerumani .

Lakini swali la pili, ni kweli alishazungumza hata katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Bunge la safari hii amezungumza pale kwamba, tuwe na Mfuko Maalumu wa kuweza kupata mafunzo kwa timu yetu ya Taifa ili kupunguza mzigo kwa Serikali. Utaratibu huo tunauandaa ili tuwe na Mfuko Maalum kwa ajili ya Timu yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Na. 418

**Utekelezaji wa Mipango/Mikakati ya Maendeleo nchini**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa kujenga uchumi wa kisasa na kuwawezesha wananchi kiuchumi ndio malengo makuu ya maendeleo ya Taifa letu; na kwa kuwa Serikali inalo jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Mikakati mbalimbali iliyoandaliwa na Serikali kwa ajili hiyo kama vile MKUKUTA, MKURABITA, Mpango Mkuu wa Kilimo *(ASDP)*, Mpango unaosaidia *ASAP (PEDEP)*, *DADPs*, *TASAF*, *SELF*, *EPZ* na *Mini-Tiger 2020*, kiasi cha shilingi bilioni moja kwa kila Wilaya; na kwa kuwa walengwa wakuu wa mipango/mikakati hiyo mbalimbali ni wananchi wote na Taifa kwa ujumla na uelewa wa wananchi hao juu ya mipango hiyo ndio itakayofanikisha malengo yote:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani wananchi walengwa katika ngazi za vijiji na taasisi wameelimishwa kuhusu mipango/mikakati hiyo na ni kwa kiasi gani wameshiriki na kunufaika na mipango hiyo?

(b) Je, ni mafanikio na matatizo gani yamepatikana hadi sasa katika utekelezaji wa mipango na mikakati hiyo na Serikali ina mipango gani ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na hatua za maboresho ili kuleta ufanisi?

(c) Je, ki-halisi ni wanajamii wangapi, vikundi na taasisi zao ngapi zimekwisha faidika na mipango hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali ilipitisha Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) mwezi Februari, 2005, kama utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Mkakati huu ni mwendelezo wa Mkakati wa awali, uliotekelezwa kati ya mwaka 2000 - 2004, uliojulikana kama Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Katika kipindi cha Mkakati wa awali na huu wa sasa, Mikakati ya Kisekta na Programu mbalimbali zimebuniwa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa malengo ya Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Mikakati hiyo ya Kisekta, pamoja na Programu Maalumu, ndizo hizo zinazotajwa na Mheshimiwa Mbunge. Hivyo, napenda kusisitiza kuwa Mikakati ya Kisekta, pamoja na Programu Maalumu ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na ni sehemu ya Mkakati wa muda wa kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya awali, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na asasi zisizo za Kiserikali, imeendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kwa njia ya semina, redio, magazeti na televisheni kuhusu malengo ya mikakati na mipango ya maendeleo iliyobuniwa ili

washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mikakati na mipango hiyo. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, vikundi 388 vya wenye biashara ndogo ndogo vimenufaika na mafunzo ya ujasiriamali na urasimishaji kupitia Mpango wa MKURABITA, Mradi wa *TASAF*, uliotoa mafunzo ya usimamizi wa miradi kwa wataalamu 10,077 katika ngazi za Halmashauri, Vijiji na Mitaa. Programu ya *ASDP* ilitoa mafunzo ya udhibiti wa nzi wa matunda kwa wataalamu 93 na wakulima 800 wa Wilaya za Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam. Aidha, wananchi wameshiriki kikamilifu katika kuibua na kubuni mipango yao ya maendeleo kupitia mfumo unaofahamika kama vikwazo na fursa za Maendeleo *(Obstacles and Opportunities for Development – O & OD).* Mfumo huu unahakikisha kuwa, Mipango ya Kitaifa inaibuliwa kutoka ngazi za chini kwa kuzingatia kero za wananchi, fursa na vikwazo vilivyopo.

Wananchi wengi wamenufaika na Mikakati na Mipango hii ya Serikali. Mifano ya wazi ya mafanikio hayo ni pamoja na upanuzi wa elimu ya msingi na sekondari, huduma za afya vijijini, barabara na madaraja. Hadi mwaka 2006, idadi ya wanafunzi walioandikishwa shule ya msingi ilifikia asilimia 96.1 toka asilimia 90.5 mwaka 2004, zahanati 225 zilijengwa nchini kote, huduma ya maji safi vijijini imeongezeka hadi asilimia 56 mwaka 2006 kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005. Katika eneo la Sekondari za Kata, shule 1,084 zilikuwa zimejengwa na kufunguliwa ilipofika Mei 31, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mikakati na Programu za Maendeleo umekuwa na mafanikio pamoja na kuwepo changamoto kadhaa. Pamekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na huduma za jamii (elimu, maji na afya) kama nilivyoeleza katika jibu (a). Aidha, pamekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika miundombinu ya barabara hasa vijijini, ambapo kwa mwaka 2006 barabara zenye urefu wa kilomita 3,181 vijijini zilitengenezwa. Aidha, wananchi wamefaidika na mikopo yenye masharti nafuu, mfano hadi mwezi Machi, 2007, Mradi wa *SELF* umetoa mikopo jumla ya shilingi bilioni 10.511 kwa wananchi 52,750, kati ya hao asilimia 80.1 ni wanawake. Aidha, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP),* imeendeleza eneo la kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 9,557. Mradi wa *TASAF* nao umeidhinisha jumla ya miradi 2,561 yenye thamani ya shilingi 36,591,798,931; kati ya hiyo miradi 1,974 ni ya maendeleo ya jamii, 162 ni ya kaya zenye uhaba wa chakula na 425 ni ya watu wa makundi maalumu. Kwa upande wa MKURABITA, hadi sasa ni vijiji saba vya Wilaya ya Handeni vimepata vyeti vya vijiji kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu hii umenufaisha wananchi takriban wote katika nchi yetu kwa namna mbalimbali na kama ilivyoelezwa hapo juu.

**NAIBU SPIKA:** Swali refu linaleta watu wasi-*pay attention,* majibu marefu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza ni kwamba, pamoja na jitihada hizo nzuri zilizofanywa, bado kuna malalamiko mengi sana ya wananchi katika sehemu mbalimbali kama ambavyo Mkutano huu wa Bunge umeshashuhudia kwamba, sehemu nyingi hawana uelewa na wanapata vikwazo vingi sana katika kufaidika na miradi hii. Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa vizuri kuwa na ratiba ya mipango hii iliyo wazi ambayo inaonesha kwamba lini watafika kwa Maofisa wa MKURABITA na mengineyo na kuwaondolea vikwazo vya utekelezaji kama watendaji wabovu kama vile mabenki yalivyo na matatizo?

Swali la pili, kwa kuwa ushindani mara nyingi unasisimua maendeleo. Je, Serikali haifikirii kwamba itakuwa ni vizuri kuweka malengo mahsusi kwa shughuli hizi mbalimbali licha ile ya *B & B* ili wananchi waweze kuhamasika zaidi washindane, watendaji zaidi ya *OPRAS* waweze kufanya kazi vizuri zaidi ili kuweza kuleta msukumo na maendeleo yanayotakiwa katika utekelezaji wa mipango yote wa miradi hii? Asante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kipindi chote hiki, imefanya juhudi kubwa ya kuweza kuwaelimisha wananchi kupitia redio, semina na warsha. Lakini ni kweli pia iko nafasi kubwa ya kuweza kuendelea kutoa elimu hii kwa wananchi na hii kama ambavyo ilielezwa katika Hotuba ya Waziri wa Mipango ya bajeti, inaendelea na itaendelea katika kipindi hiki cha fedha kinachokuja. Tutaona na tutatembelea katika mikoa na wilaya kuelimisha zaidi wananchi.

Kuhusu swali la pili la ushindani ni kweli ushindani unasaidia na hata katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tunahimizwa kuwashindanisha wakulima wetu. Kwa hiyo, ningehimiza katika Wilaya kuwe na Mipango Maalum ya kuwashindanisha wananchi katika maeneo mbalimbali. Ni jambo ambalo linaweza likafanyika kutoka katika ngazi ya Vijiji, Wilaya na Mikoa.

Na. 419

**Ruhusa ya Kurudia Daraja la Saba**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba huwa na umri mdogo; na kwa kuwa wengi wao huwa hawapati nafasi za kuendelea na masomo ya sekondari kutokana na kutokomaa kiakili: Je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa wanafunzi hao waruhusiwe kurudia Darasa la Saba ili kuwapa uwezo zaidi wa kukomaa kiakili kama ilivyokuwa miaka ya nyuma?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, wanafunzi hutakiwa kuanza Darasa la Kwanza wakiwa na umri wa miaka saba na hivyo kuhitimu Darasa la Saba wakiwa na umri wa miaka 13. Umri huu, unakubalika kimataifa kwa kuwa katika umri huo, mwanafunzi anakuwa amekomaa kiakili. Kwa sasa utaratibu wa kuwaruhusu wanafunzi wanaokosa nafasi ya kiujiunga na Elimu ya Sekondari kukariri Darasa la Saba haupo, kutokana na uwezo mdogo wa Serikali. Serikali itajitahidi kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuongeza ufaulu. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi, Taasisi za Dini na watu binafsi, itaendelea na juhudi za kuongeza nafasi za Shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi ili idadi kubwa ya wanaofaulu Darasa la Saba waweze kupata nafasi za kuendelea na masomo ya sekondari na wengine wajiunge na vyuo vya ufundi, kujifunza stadi mbalimbali za maisha na ujasiriamali ili waweze kuyakabili maisha vizuri zaidi.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanafunzi wanaomaliza Darasa Saba wanakuwa na umri mdogo kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, umri wa miaka 13, kitu ambacho hawawezi wakajitegemea kimaisha na matokeo wanakuwa wanaishia mtaani; na kwa kuwa hizo shule za ufundi hazijawa tayari na idadi ya wanafunzi inaongezeka; je, Serikali ina mipango gani ya dharura ya kupunguza idadi hiyo ya wanafunzi ambao wanamaliza Darasa la Saba ambao hawajitegemei?

La pili, kwa kuwa shule za sekondari zinaongezeka na kwa kuwa nafasi za wanafunzi zitaongezeka sasa kujiunga na Serikali; je, Serikali haioni kwamba shule ya sekondari ndiyo iwe elimu ya lazima kwa wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa namna ya kipekee anavyofuatilia masuala ya elimu.

Baada ya hapo naomba kumjibu kwamba ni kweli umri huo ni mdogo, wanafunzi hao wanakuwa hawawezi kujitegemea ndiyo maana Serikali kwa kutambua hilo, imeanzisha somo la stadi za kazi ndani ya mtaala wa elimu ya msingi. Kwenye stadi za kazi kuna mambo machache ambayo yakipatikana au yakitolewa na kupokelewa kwa wanafunzi, wataweza kuanza maisha yao vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, Serikali itangaze sasa kwamba sekondari iwe na elimu ya lazima. Naomba niseme, bado hatujafika kwenye uwezo huo sawa sawa, maana unahitaji maandalizi makubwa, mipango mingi na hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge naamini kabisa tutafika huko siku si nyingi.

Na. 420

**Hitaji la Umeme Busanda**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni kati ya nyenzo muhimu katika kuhamasisha maendeleo na kukuza uchumi wa jamii; na kwa kuwa katika Jimbo la Busanda kuna shughuli nyingi zinazohitaji umeme mfano uchimbaji madini, shule za sekondari kila Kata na viwanda vya kuchambua na kusindika pamba *(gineries):-*

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika maeneo ya Nyakagwe, Bukori, Nyamalimbe, Kamena, Nyarugusu, Busanda, Rwamgasa, Kaseme, Katoro hadi Butundwe ili kuhamasisha maendeleo hayo?

(b) Je, mpango wa mradi wa kupeleka umeme Geita, Katoro, Biharamulo, Kibondo na Chato kutoka Kakola *(Kahama Mine)* umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa umeme katika kuleta maendeleo kwa wananchi, Serikali kwa msaada wa Serikali ya Sweden, imekamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kupanua Gridi ya Taifa kufikia Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera, iliyoko Kaskazini – Magharibi mwa nchi. Mradi huu unaitwa *North West Grid Extension.* Mradi huu pia utahusisha usambazaji wa umeme wa Gridi katika miji midogo na vijiji kwenye mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Jimbo la Busanda na mengine yaliyo Wilayani Geita na Bukombe, yamejumuishwa katika upembuzi yakinifu wa Mradi huo. Maeneo ya Bukoli, Kamena, Nyarugusu, Rwamgasa, Kaseme na Katoro, yatanufaika chini ya mradi huu mara utekelezaji wa mradi utakapoanza. Hata hivyo, maeneo ya Nyakagwe, Nyamalimbe na Busanda, hayakuhusishwa kwenye upembuzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya upembuzi yakinifu uliofanyika, yatatumika katika majadiliano ya kuomba fedha kutoka Serikali ya Sweden na wafadhili wengine. Mara fedha zitakapopatikana, Serikali itatoa ratiba ya utekelezaji wa Mradi wa *North West Grid Extension.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi F. Rwiromba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya usambazaji umeme kwenye maeneo ya Bukori, Kamena, Nyarugusu, Rwamgasa, Kaseme, Katoro na Butundwe, itatekelezwa baada ya

Serikali kupata fedha za utekelezaji wa Mradi wa *North West Grid Extension,* kwa kuzingatia mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa ya upembuzi yakinifu.

Aidha, Serikali italiagiza Shirika la *TANESCO* kuanza mipango ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye maeneo ya Nyakagwe, Nyamalimbe na Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji ya Geita, Katoro, Biharamulo, Kibondo na Chato, imejumuishwa kupatiwa umeme chini ya Mradi wa *North West Grid Extension*. Hatua iliyofikiwa ni ya kufanyiwa upembuzi yakinifu katika maeneo hayo. Mazungumzo na Serikali ya Sweden yanaendelea ili kupata fedha za utekelezaji wa mradi huu.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa bado fedha zinatafutwa ili *project* hiyo aliyoisema iweze kutekelezwa na inawezekana inaweza ikachukua muda mrefu; na kwa kuwa umeme ulioko Geita una uwezo wa kupelekwa umbali kilomita 150 na maeneo niliyoyataja hayazidi kilimita 30; je, haoni kwamba sasa ni vyema *TANESCO* ikaanza kazi kwa kuanza kusogeza angalau umeme katika maeneo hayo hasa ukiangalia Nyarugusu kuna mgodi mkubwa ambao unatarajiwa kufunguliwa pale, ambao utazalisha fedha nyingi kwa ajili ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba, ingewezekana kwa kiasi fulani umeme uliopo Geita kuweza kufika kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema. Lakini tunachofanya sasa hivi katika mradi huu, hatuangalii maeneo ya Jimbo la Mheshimiwa Mbunge tu peke yake, mradi huu utajenga fursa kuvihudumia vijiji na maeneo mengi zaidi kuliko kuhudumia katika eneo moja tu ambalo tunaamini kwamba, kwa kufanya vile tutakuwa tumewanyima huduma wananchi wa maeneo mengine.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine pia, tuvute subira tunafahamu ni kilio cha wananchi wengi, lakini pia ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba, utakapokamilika mradi huu, maeneo mengi zaidi yatafaidika. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane tuwashauri wananchi wavumilie wakati tunasubiri utekelezaji wa mradi huu ambao utakuwa na manufaa kwa wananchi wengi zaidi, kuliko ambavyo ingeweza kufanyika kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anapendekeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda wa mwanzo kutokana matangazo ya kuwasilisha nyaraka lakini maswali mengine yalikuwa marefu. Sasa nina matangazo ya Wageni. Nadhani kuna Wabunge wengine hawajawahi kusikia maelezo yetu kwamba, wageni wanatakiwa kupelekwa majina yao Ofisi ya Bunge siku moja kabla ya siku ya leo na yawe yamechapishwa sio vikaratasi. Kwa hiyo, wanaoleta vikaratasi hawatangazwi wageni wao. Kwa hiyo, nina wageni wafuatao, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan ana wageni wake; Ndugu Fatuma Haji, Mjumbe wa Baraza Kuu la Wazazi kutoka Zanzibar na Ndugu Catherine Peter, Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Zanzibar, karibuni mlikuwa kwenye kikao.

Mheshimiwa Haroub Said Masoud ana mgeni wake anaitwa Ndugu Gadish Rashid kutoka Dubai. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Magreth A. Mkanga hao ni Mwalimu Zitabata Manangwa na Mwalimu Magali Mocha, karibuni sana walimu. Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu naye ana wageni wake; kuna Ndugu Emmanuel Bongowe Limbu, mtoto wake, akifuatana na ndugu yake, Ndugu Getrude Limbu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa John P. Lwanji, wao ni Ndugu Ally Kilangilo, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Mkoa wa Singida, kuna Mheshimiwa Juma Mgulu, Mtendaji wa Kata ya Ipate, halafu na Mheshimiwa Magwe Kisiba, Katibu wa CCM Tawi la Kasaramba, karibuni sana.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Janeth B. Kahama, yuko Bibi Martha Mtebe, dada yake, amefuatana na Bibi Rahma Bomani na Bibi Grace Kisie. Halafu tuna wanafunzi 57 kutoka Shule ya Sekondari Msalato, wasimame wote na walimu, karibuni sana. Nategemea mnafanya bidii huko shuleni. Tuna wanafunzi 40 wa kutoka *CTS Vocation Training Centre Dodoma* na wao wasimame wote na walimu, karibu sana. Tuna wanafunzi 26 kutoka Chuo cha Ulimu, *Theresian Seminary Dodoma*, kama wapo pia tunaomba wasimame, asante sana karibuni walimu. Tuna wageni wa Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, hawa ni Mzee Paul Sozigwa na mke wake, naomba wasimame. Mzee mashuhuri tumefurahi kukuona baada ya muda mrefu. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, ambao ni Ndugu Khamis Hussein, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Unanilwa, Wilaya Kasulu. Halafu Ndugu Meshali Henda, Mkuu wa Uchumi, Fedha na Mipango CCM, Kata ya Mnanila Kasulu, karibuni ndugu zangu. *(Makofi)*

Sasa mjiandae ninyi ambao ni wapenzi wa Yanga na Waheshimiwa Wabunge akiwepo, haya basi mshangalie. Tunao wachezaji wa Yanga wakiwa na Kombe la *TUSKER,* walioshinda wiki iliyopita Mjini Mwanza, wakiongozwa na mkuu wa msafara, wasimame wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa tunawashangilia kwa sababu wamepeperusha bendera yetu katika mashindano hayo. Kwa hiyo, tunawapongeza sana na tunajivunia ushindi huo na tunafarijika kuwa nanyi, mmefanya vizuri na kuweza kuiweka nchi yetu katika hali ya ufanisi mzuri zaidi na sio kichwa cha mwendawazimu tena. *(Makofi)*

Kati ya hao wachezaji kuna mdogo wake Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, yuko hapo hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa William H. Shellukindo, anawafahamisha Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati, ghorofa ya nne chumba namba 432.

Halafu Mheshimiwa William J. Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anaomba kuwatangazia wajumbe wake kwamba, leo saa tano asubuhi katika

ukumbi 219 ghorofa ya pili kutakuwa na kikao. Lakini Waheshimiwa Wabunge, saa saba tutakuwa na Kamati ya Kanuni, kwa hiyo, haturuhusu watu wengine wakafanye mkutano mwingine. Hao waende saa saba katika chumba 219, tutakuwa na kikao cha Kanuni.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, yeye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, anawatangazia Makamu Wenyeviti wote wa Kamati kwamba, wakutane chumba Namba 31, muda hakutaja itakuwa saa saba. Katibu wa Umoja wa Wanawake wa CCM kutoka Zanzibar, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, anaomba tuwatangazie Wajumbe wa Umoja huo, kutakuwa na mkutano na wenyewe saa saba chumba 231, saa tano hamtakwenda tuna kazi ya pamoja. Halafu Katibu wa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, anapenda kuwatangazia wanachama wa CCM waliopo humu kwamba, leo wote wapite Ofisi ya Chama, Jengo la Utawala chumba 106, kupokea maagizo muhimu kuhusu Mkutano Mkuu, kutakuwepo na mtu kule wakapokee maagizo muhimu kuhusiana na Mkutano Mkuu.

Tangazo la Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Bunge baada ya shughuli zilizopo kwenye *Order Paper* hii na ni Miswada kusomwa kwa mara ya kwanza, tutakuwa kwa leo hatutaendelea na Shughuli rasmi za Bunge. Tutaahirisha kikao, mimi nitakwenda kubadilisha nguo halafu tutapiga kengele saa tano ili mrudi hapa, tuendeshe kama warsha ama semina kwa ajili ya kanuni zetu. Kanuni zetu tunataka kuzifanyia mabadiliko makubwa sana. Kwa hiyo, kabla hatujayaleta Bungeni rasmi, tunapenda Wabunge washiriki kwa kutoa mawazo, kujadili kwa uhuru zaidi. Tukiingia kujadili hapa kiutaratibu inakuwa vigumu sana kufanya mabadiliko yanayostahili na kuweza kubishana ama mtu kusema zaidi ya mara moja.

Lakini tukiwa na *workshop* tunaweza kuzungumza kwa mara nyingi hata ukaweza kutoa hoja yenye uzito, tuweze kuingiza ama kupunguza kitu fulani. Kwa hiyo, tutakuwa na hili zoezi leo na kesho pia kwa sababu ni mabadiliko makubwa, kwa hiyo tutakuwa na kazi hiyo. Mimi nitatoka, tuaahirisha kikao kidogo, tutapiga kengele mtarudi tutafanyia hapa hapa. Wakati huo wageni wowote wa nje hatuwakaribishi, kwa sababu ni kazi yetu ya ndani. Kwa hiyo, wageni wote tutawaomba waje tena kesho kwenye kipindi cha maswali.

Nategemea Waheshimiwa Wabunge wote mtakuwepo, kwa sababu ni muhimu. Kwa wale wanaozijua vizuri Kanuni za Bunge, kuendesha Bunge kunakuwa rahisi, kwa mtu asiyejua hapa ataona kama anaonewa tu, lakini kumbe hazijui kanuni. Wakati mzuri wa kuzijua Kanuni ni sasa wakati wa kutengeneza, ukizujua basi zinakaa vizuri, baadaye zikiwekwa kuwa ni sheria. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa manufaa yako wewe kama Mbunge ni vizuri ukashiriki katika kutengeneza kanuni vizuri zaidi. Kwa hiyo, tunaendelea na shughuli inayofuata.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Wahandisi wa Mwaka 2007 *(The Engineers Registration (Amendment) Bill, 2007)***

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 *(The National Construction Council (Amendment) Bill, 2007)***

**Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Afya ya Mazingira wa Mwaka 2007 *(The Enviromental Health Practitioners (Registration) Bill, 2007)***

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2007 *(*The *Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2007)***

**Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 *(The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007)***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Miswada yote hii inategemewa kuwa katika *Pigeonholes*, muweze kufanya marejea huko halafu baadaye ndipo itapokuja katika Bunge linalokuja. Kwa hiyo, Miswada hii itakuwepo kwenye *pigeonholes* zenu, kwa hiyo ni *public*.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwamba, leo tunamalizia maswali kesho pia tutaingia maswali halafu tunaendelea na shughuli zetu. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04:22 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*